JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
MKOA WA NJOMBE
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE

Shule ya Sekondari Ipepo,
S.L.P.186,
MAKETE.
Simu:0753026716

Kumb Na.IPPSS/J.INS/2020 05/12/2020

Jina la mwanafunzi……

S.L.P……

YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IPEPO WILAYA YA MAKETE MKOA WA NJOMBE MWAKA 2021.

1.0.UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka 2021.Shule ya Sekondari Ipepo ipo Wilaya ya Makete,Tarafa ya Ukwama,Kata ya Ipepo,Kijiji cha Ipepo kilometa 46 mashariki kusini kutoka Makete mjini. Shule ni ya mchanganyiko wavulana na wasichana pia ni ya hosteli kwa jinsia zote.

Muhula wa kuanza masomo unaanza **tarehe 11.1.2021**.Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **11.1.2021**.Baada ya hapo taratibu za kisheria zitafwatwa kwa mzazi/mlezi yeyote atakaye kuwa amemchelewesha mwanafunzi kuripoti kwa muda husika.Unashauriwa kumwandalia mahitaji yote mwanao kabla ya tarehe tajwa hapo juu ili kuepusha usumbufu.

2.0.MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1.SARE ZA SHULE.

a)Sare ya shule kwa **WAVULANA.**

-Shati mbili nyeupe mikono mirefu zisizobana mwili.

-Suruali mbili rangi nyeusi na kaki.(kitambaa aina ya **istimu**)

-Aje na tai mbili rangi nyeusi na kaki.

-Soksi pea tatu (3) rangi nyeusi .

- Shati pamoja suruali isiyobana rangi ya damu ya mzee .

KWA WASICHANA.

-Shati mbili (2) nyeupe mikono mirefu zisizobana mwili.

-**Suruali mbili** na **sketi mbili** mshono wa **RINDABOKSI** kitambaa aina ya **istim nzito** kwa rangi ya **zambarau** na **nyeusi** zisizobana.

-Skafu mbili kubwa rangi ya **zambarau** na **nyeusi**.

-Soksi pea nne (4) rangi nyeupe

-Gauni rangi ya damu ya mzee isiyobana kitambaa aina ya **istimu nzito**

b)MAHITAJI YA JUMLA KWA MWANAFUNZI WOTE

Wavulana na Wasichana.

-Sweta mbili(2) rangi ya bluu-mshono wa V shingoni.

-Viatu vyeusi pea mbili(2) vya ngozi vikiwa na kamba .

-Track suit moja **rangi nyeusi** isiyobana mwili.

-Shuka mbili(2) rangi ya **bluu bahari** na blanketi mbili(2).

-T-shirt moja rangi ya **njano** isiyo bana.

-Godoro 2.5x6 la mwanafunzi.

-Sanduku la bati au lakuchongwa lenye kufuli.

-Ndoo mbili ndogo za lita kumi.

-Jembe **jipya** lenye mpini,kwanja na panga.

-Daftari kubwa kumi (**3quire counters**),rimu kwa ajili ya mitihani ,rula,mkebe moja mkubwa wenye vifaa vyote,pamoja na mfuko wa kuchukulia madaftari pamoja na kalamu/peni za kutosha.

-Nguo za kujisitiri sehemu muhimu kama binadamu(za ndani) zakutosha.

c)SARE YA MICHEZO.

Wavulana:-Raba imara pea moja,fulana na bukta rangi ya kijani isiyobana,soksi pea mbili rangi ya njano.

Wasichana:-raba imara pea moja,fulana na bukta rangi nyeupe isiyobana,soksi pea mbili rangi nyeupe.

3.0.MAJUKUMU YA MZAZI/MLEZI.

Ni kuhakikisha kuwa huduma zifuatazo zinapatikana kwa mwanafunzi na kwa wakati:-

Sare za shule na michezo ,vifaa vya kujifunzia kama daftari na kalamu,chakula kwa mwanafunzi,matibabu,vifaa vya kulalia(godoro,shuka na blanketi) na mahitaji ya kibinadamu(nguo za ndani za kutosha).

Mchango wa chakula kwa mwaka ni kama ifuatavyo:-

Mahindi debe nane(8), maharage debe 3, mafuta lita 2, sukari kilo 6, sabuni vipande viwili, chumvi kilo 4 pamoja na tsh 100,000/= .

NB:Mchango wa chakula utaletwa wakati wa kuripoti shuleni na kupokelewa na kamati ya chakula ya wazazi.

Muhimu:-Mzazi/Mlezi soma kwa umakini maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu kabla au ifikapo tarehe **11/01/2021** siku ya kuripoti shuleni, kinyume na hapo **mzazi/mlezi utawajibika kwakuto mkamilishia mahitaji mwanao.**

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI IPEPO !

Dionis V.Mgina

MKUU WA SHULE

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na .10 ya mwaka 1995. Aidha,inazingatia miongozo yote inayo tolewa na Wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia na Ufundi,yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu.unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:-

a)Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b)Mahudhurio mazuri katika kila shunguli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

c)Kushiriki kwa makini katika maandalio ya jioni(preparation).

d)Kuwahi katika kila shuguli za shule na nyinginezo utakazopewa.

e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

f)Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.

g)Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

h)Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

i)Kutunza mali za umma.

j)Kuwajibika kwenye michezo,mazoezi mbalimbali na mchakamchaka shuleni.

k)Kuongea lugha ya kiingereza uwapo shuleni.

3.2.Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

a)wizi au Kuwa na simu ya mkononi .
b)Uasherati , ushoga na Ubakaji,uchonganishi na mawasiliano yasiyo fuata taratibu.
c)Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kubeli na kadhalika.
d)Kupigana au kupiga au Kukataa adhabu kwa makusudi.
e)Kuharibu kwa makusudi mali ya umma au mali ya mwanafunzi mwenzako.
f)Kudharau bendera ya taifa.
g)Kuwa mjamzito au kusababisha mimba au Kuoa au kuolewa au Kutoa mimba.
k)Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

b)FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI NA MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO,FUJO NA MAKOSA YA JINAI.

Mimi----------(jina la mwanafunzi) niliye zaliwa mwaka ----------
kijiji cha----------niliyesoma shule ya msingi----------
nina mzazi/mlezi aitwaye----------shughuli ya mzazi/mlezi ni----------

Mimi mwanafunzi nimesoma na kuelewa sheria na kanuni zote za shule **sitashiriki kwa namna yeyote katika migomo,fujo,kushawishi wengine kufanya fujo au migomo na makosa ya jinai.Itakapo thibitika kushiriki kwa namna yeyote hatua kali zichukuliwe**.Nitashirikiana katika kuhakikisha nafwata sheria,kanuni na taratibu zote za shule hii zitazonifanya nifanikishe ndoto za kumpata ELIMU kwa faida yangu na taifa kwa ujumla.

Jina la mwanafunzi----------

Sahihi ya mkataba wa mwanafunzi----------tarehe----------

c)FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA,KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE.

Mimi mzazi au mlezi----------
wa mwanafunzi----------
nakiri na kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule na kutii kwa wakati.**Pia nipo tayari na kuhakikisha nampatia mwanafunzi mahitaji yote kwa wakati**.Kinyume na hapo nitapaswa kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria.

Jina la mzazi/mlezi wa mwanafumzi----------

Sahihi ya mzazi/mlezi ya makubaliano----------tarehe----------

d).SEHEMU YA MGANGA.

MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING

IPEPO SECONDARY SCHOOL

(*REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION)*

This form must be completed by a government medical officer.

Name of student----------

Age----------sex----------

The above named student has been examined in respect of

a)PREGNANT TEST (FOR GIRLS ONLY)----------

b)STOOL----------

c)URINE----------

d)CHEST----------

e)BLOOD----------

f)EYES----------

g)EARS----------

h)OTHER FINDINGS----------

I am certified that the above student is fit/not fit for pursuing secondary studies at IPEPO SECONDARY SCHOOL.

---------- ----------

SIGNATURE DATE

---------- ----------

DESIGNATION and OFFICIAL STAMP STATION